

Mfungwa anaamini anakidhi vigezo vya msamaha anaweza kuiomba Bodi kuachiwa kwa msamaha.

Baada kujiridhisha mfungwa anakidhi masharti, Bodi itawasilisha kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya magereza mapendekezo ya kuachiwa mfungwa husika. Waziri ndiye mwenye dhamana ya uamuzi.

4.4 Sheria ya Magereza, Sura ya 58

Inspekta Jenerali wa Magereza ana madaraka kisheria kupunguza theluthi ya vifungo kwa wafungwa walioonesha tabia njema isipokuwa kwa wafungwa waliofungwa chini ya Sheria ya Kiwango cha Chini cha Adhabu au vifungo vya maisha.

Ofisa Mfawidhi wa Gereza, iwapo ameridhika kwamba, mfungwa aliyepo kwenye gereza analosimamia amekidhi vigezo vya kutumikia adhabu katika jamii chini ya Sheria ya Huduma kwa Jamii, atamjulisha. Endapo mfungwa ataridhia masharti yaliyoainishwa, Ofisa Mfawidhi wa Gereza atawasilisha suala hilo katika mahakama yenye mamlaka ili itoe amri kwa mfungwa husika kutumikia jamii.

4.5 Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20

Sheria inaruhusu mshtakiwa, pamoja na wakili wake au mtu mwingine anayesimama kwa niaba, kuingia makubaliano ya kukiri kosa na Mkurugenzi wa Mashtaka ili kulipa faini au fidia itakayokubaliwa. Lengo likiwa ni kupunguziwa makosa au adhabu, kulipa faini au fidia, kurejesha mali au kutaifisha mali zinazotokana na uhalifu.

Makubaliano ya kukiri makosa yatakuwa na nguvu ya kisheria baada ya kusajiliwa katika mahakama. Ambayo itamtia hatiani mshitakiwa na kutoa amri kama ilivyokubaliwa katika mkataba.

Kwa maoni, wasiliana na Tume kupitia anuani ifuatayo:

**Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,
Jengo la Taaluma Na. 1, Barabara ya Mkalama
S.L.P. 1718
DODOMA, TANZANIA**

Barua pepe: lrct@lrct.go.tz
Tovuti: www.lrct.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



ADHABU MBADALA

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kufanya mapitio na kutathmini utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kitekinolojia.

2.0 Adhabu

Kosa la jinai ni tendo lolote ambalo limekatazwa kwa sheria. Mtu anayepatikana na hatia ya makosa ya jinai huadhibiwa. Adhabu kwa makosa ya jinai ni kifungo gerezani kwa muda maalum au maisha, kunyongwa hadi kufa, kifungo cha nje, kifungo cha masharti, viboko, fidia na faini. Adhabu mbadala ni adhabu zisizojumuisha adhabu ya kunyongwa na vifungo vya magerezani.

3.0 Madhumuni ya Adhabu Mbadala

Madhumuni ya adhabu mbadala ni pamoja na kuwafanyia urekebu wafungwa wakiwa nje ya magereza, kupunguza msongamano wa wafungwa, kupunguza gharama za kuhudumia magereza, kuwezesha wafungwa kuhudumia familia zao wakiwa wanatekeleza adhabu zao, na kujumuisha

jamii katika usimamizi na urekebu wa wahalifu.

4.0 Mfumo wa Sheria Zinazosimamia Adhabu Mbadala

Sheria mbalimbali zimetunga ili kuwezesha utekelezaji wa adhabu mbadala katika mfumo wa haki jinai. Sheria hizo ni:

4.1 Sheria ya Huduma kwa Jamii, Sura ya 291

Sheria inatoa adhabu kwa mfungwa kufanya kazi za umma bila malipo kwa muda maalum. Mtu yeyote aliyehukumiwa kifungo kisichozidi miaka 3 pamoja na, au bila faini, au kifungo kinachozidi miaka 3, mahakama inaweza kutoa amri kupitia Sheria hii mtu huyo atumikie adhabu ya hudumia jamii.

4.2 Sheria ya Uangalizi wa Wahalifu, Sura ya 247

Sheria inaweka masharti ya uangalizi wa mhalifu na kumweka mhalifu chini ya amri ya uangalizi wa Afisa Uangalizi kwa kipindi kisichopungua mwaka 1 na kisichozidi miaka 3 ambacho anatakiwa asifanye kosa lolote.

Sheria inazipa mamlaka mahakama za mwanzo, Wilaya, hakimku mkazi na Mahakama Kuu kutoa amri ya uangalizi baada ya kujiridhisha kuwa amri hiyo inafaa kutolewa.

Sheria imeweka masharti ya kuzingatiwa kabla ya mahakama kutoa Amri ya Uangalizi kwa mhalifu ambayo ni umri, tabia, mwenendo wa maisha, afya ikiwa ni pamoja na afya ya akili, mazingira anayoishi, aina ya kosa alilotenda na mazingira ya kutendeka kwa kosa. Amri hii hutolewa kwa mhalifu iwapo anaridhia masharti yote yatakayoanishwa kutotenda makosa ya uhalifu awapo nje ya kifungo chini ya uangalizi. Endapo mhalifu atakiuka masharti yaliyowekwa atafutiwa amri ya uangalizi na atahukumiwa kifungo kulingana na kosa alilotenda awali.

4.3 Sheria ya Bodi ya Msamaha kwa Wafungwa, Sura ya 400

Mfungwa anayenufaika na msamaha, anatakiwa awe amefungwa kifungo kuanzia miaka minne na kuendelea na hatumikii kifungo cha maisha, hakufungwa kwa makosa ya uhalifu wa kutumia silaha, madawa ya kulevyu, ubakaji au unajisi. Masharti mengine ni kifungo chake kutowekwa katika huduma kwa jamii; awe ametumikia theluthi ya kifungo na ameonesha tabia njema wakati akitumikia kifungo kabla ya kuwekwa kwenye msamaha.